**NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO**

**"KABUMBU AFRIKA - NI ZAIDI YA MCHEZO!"**

**EPISODE TWO: "Mchezo msafi:Mchezo mchafu"**

**Mwandishi: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

**Orodha ya wahusika kipindi cha pili:**

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S FLAT**
- Safina (mke, 13)
- Shangazi Lily (mke, 33)

**SCENE TWO: TAMBARARE CITY LATE AFTERNOON**
- Chedede (mume,14)
- Komora (mume,14)
- mhudumu wa kike (mke, 20)

**SCENE THREE: AT THE HOTEL**
- Jonathan (mume,15)
- MHE.Makemba (mume, 55)
- Metogba (mchezaji wa kulipwa - mume, 28)

**SCENE FOUR: LATE EVENING AUNT LILY'S FLAT**
- Safina (mke, 13)
- Shangazi Lily (mke, 33)

**INTRO:**

**1. NARRATORI**:Nawasalimu tena na karibuni katika kipindi hiki cha Noa Bongo-Jenga Maisha yako ,kwenye makala ya pili ya **"Kabumbu Afrika - ni zaidi ya mchezo!".** Katika kipindi kilichopita, tulimuacha chokoraa Chedede akikimbia kumuelezea Komora kuhusu taarifa za kliniki ya soka alizosikia kwenye habari za michezo.Safina naye alikuwa tayari amewasili kwa shangazi yake na kumkabidhi barua aliyoandikiwa na mamake - na Jonathan alikuwa tayari amearifiwa na babake. aliye mwanasiasa maarufu, kuhusu kliniki hiyohiyo. Baki nasi ubaini kitakachotokea katika kipindi hiki cha pili **"Mchezo msafii na mchezo mchafu"**.Tuanzie kwa Shangazi Lily anayeanza kuisoma barua aliyoandikiwa na dadake, yaani mamake Safina.

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S**

**(SAME MUSIC AS IN EPISODE ONE, LOWER VOLUME)**

2. **SFX: PAPERS BEING SHUFFLED**

3. **SHANGAZI LILY:** Sasa, ngoja tusikie dadangu anasemaje... **(starts to read letter loudly)** Mpenzi Lily, nataraji barua hii itakupata ukiwa buheri wa afya. Ni kitambo tangu... blah blah blah... **(gets to the end**) na kwa sababu hatuna uwezo wa kumpeleka Safina shuleni, au kutimiza mahitaji yake, tumeona ni vyema tumlete huko jijini. Utagundua kuwa ni msichana mwenye bidii sana, pia anapenda kucheza mpira.Tafadhali mtunze na umchukuwe kama wako. Salamu kutoka kwetu. Mama Safina. **( short pause followed by sarcastic laugh)**

4. **SAFINA: (puzzled by her aunt's reaction)** Shangazi Lily, ni nini kinachokuchekesha? Mbona hata hukuisoma barua yote?

5. **SHANGAZI LILY:** Haya ni matani sivyo? Haya ya kuwa unapenda kucheza kandanda, matani mabaya sana, ama?

6. **SAFINA:** La, ni kweli, na sio hivyo tu, mimi ni mchezaji hodari. Nitakuthibitishia hivi karibuni. Kuna kiwanja cha mpira hapa karibu**? (proudly**) Unajua, naweza kupepeta mpira bora kuliko vijana wengi kijijini, siku moja hata nili....

7. **SHANGAZI LILY: (using a stern voice)** Eh, eh! Safina! Hebu nisikilize vizuri, tena kwa makini, nitasema mara moja tu. Mara ngapi? Moja! Hakuna cha kucheza mpira katika nyumba yangu! umenielewa? Wewe ni msichana, sijui kama hujatambua hivyo hadi sasa, na katika miaka michache ijayo utakuwa mwanamke! Soka ni mchezo wa wavulana, wavulana wajinga ambao hawana kazi ya kufanya. Isitoshe, unafikiri majirani watasema nini wakikuona ukikimbizana huku na huko na wavulana mkicheza mpira? Hutanifanya nichekwe hapa Tambarare. Sitakubali hata kidogo!

8. **SAFINA:** Lakini... lakini…

9. **SHANGAZI LILY:** Hakuna cha lakini wala walakini! Chukua mkoba wako uuweke pale pembeni. Kisha uje hapa unisaidie kutayarisha chakula cha mchana... mpira wa miguu? Ala! Michezo yote tuliyo nayo ni lazima huo? Twaelekea wapi jamani katika dunia hii?

**10. NARRATOR:** Safina hakutarajia mapokezi kama haya. Lakini kwa vile alikuwa msichana mtiifu, alikubaliana na hali halisi haraka na kuanza kusaidia pale nyumbani.Unakumbuka tangu wakati ule? Chedede naye ana ujumbe wa kumuwasilishia rafikiye Komora.Ataupokea vipi?... Tega sikio

**SCENE TWO: TAMBARARE CITY LATE AFTERNOON**

**11. SFX: VOICES OF PEOPLE TALKING,ORDERING FOOD ETC**

**12. WAITRESS: (Shouts)** Nani maharagwe na mkate!

**13. KOMORA:** Mimi! hapa! hapa!

**14. CHEDEDE: (Chedede rushes into hotel panting)** Komora! Komora! **(tries to catch his breath)** Sikiza, hutaamini..

**15. KOMORA:** Hapana. Ah ah! Huko huko, bwana mchezaji kabumbu. Hiki chakula ni jasho langu, na sikupi hata kipande cha mkate. Si wewe unaishi kwa kitu kimoja tu maishani -soka. Ulalapo - mpira, uotapo - mpira na usemapo, kwako ni mpira tu, sawa, kwa vile una njaa, basi nenda kale mpira wa miguu pia. **(giggles in a mean way)**

**16. CHEDEDE:** Sikitaki chakula chako, ijapokuwa kinavutia na kimenitia njaa na mate pia yananidondoka. Hata hivyo, sikiliza, hutasadiki niliyoyasikia dukani kwa Shah nikitazama habari za michezo kwenye runinga... walisema ya kwamba...

**17. KOMORA: (cuts Chedede short while still eating,says with full mouth)** Ngoja kidogo. Nataraji ni taarifa nzuri **(pause**) Tafadhali tuletee kijiko chengine. Haya hebu endelea sasa…

18. **NARRATOR:** Wakati Chedede akimueleza Komora aliyoyasikia kuhusu kliniki ya kabumbu, si mbali sana na pale kwenye kibanda cha chakula, gari la kifahari lilikua linaingia kwenye sehemu ya kuegesha magari pale jijini Tambarare. Mhe. Makemba na mwanawe Jonathan walikuwa ndani ya gari hilo. Jee wanamtembelea nani hapo? Kaa papo hapo ujue zaidi.

**SCENE THREE: AT THE HOTEL**

19. **SFX: CITY AMBIENCE. CARDOOR OPENS, SHUTS. ALARM BEEPS TWICE**

20. **MHE. MAKEMBA:** Jonathan, kama tulivyokubaliana garini, niachie mimi nizungumze. Labda atakapokuuliza swali ndipo umjibu. Sawa sawa?

21. **JONATHAN:** Ndio, baba, nakumbuka. Unakifahamu chumba chake?

22. **MHE. MAKEMBA:** Nakijua vizuri.Mwanangu, mimi ni mbunge.Mimi ni mheshimiwa Makemba. Kabla ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kuzuka, nilikuwa waziri wa michezo.Nahitaji kupiga simu tu. Nakijua chumba chake,muda atakaokuwa hapa. Kitu nisichofahamu ni mchezaji mwenyewe, lakini nipe muda nitajuwa. Mengine yote nayajua,hata wale watu wote atakaofanya nao kazi. Hili halitachukuwa muda..

23. **JONATHAN:** Lakini baba, je unadhani kuwa… namaanisha je ikiwa ata…?

**24. MHE. MAKEMBA:** Usiwe na wasiwasi Jonathan. Sisi ndio tunaiongoza hii nchi. Kila kitu na kila mtu yuko chini yetu ( **whispers)** hata kandanda.

**25. SFX: SLIDING DOOR OPENS,CITY AMBIENCE FADES OUT, HOTEL LOBBY ATMOSPHERE**

**26. RECEPTIONIST**: Habari za jioni, mhe. Makemba. Karibu kiti katika sehemu maalum ya wageni muhimu.Mgeni wako atakuja sasa hivi….naenda kumwita.Ungependa kinywaji chochote labda ?

**27. MHE. MAKEMBA:** La, asante nina udhuru mwengine baada ya muda usio mrefu.Sitokuwa hapa kwa muda mwingi lakini mletee kijana wangu juisi baridi…

**28. RECEPTIONIST:** Bila shaka… namfahamisha mgeni wako umefika kisha niwaletee kinywaji.Karibu sana Mheshimiwa.…

**29. SFX: DIAL TONE SOUND THEN BUTTONS BEING PUNCHED ON A TELEPHONE.**

**30. RECEPTIONIST:** Habari za jioni Kaka. Hapa ni kwenye sehemu ya mapokezi. Samahani kwa kukusumbua lakini mgeni wako amewasili, anakusubiri.

**31. METOGBA: (through telephone with a sleepy voice)**
Mgeni? Mgeni gani? Wageni ninaotarajia ni waandishi wa habari na nitakutana nao kesho... niliwaarifu kitambo kwamba sitaki kusumbuliwa hadi hapo kesho...

32. **MPOKEZI:** Naelewa, na singekusumbua ni vile tu huyu si mgeni wa kawaida…

33. **METOGBA:** Hmm… ni mgeni gani huyo basi? Sawa, mfahamishe nitamuona baada ya dakika kumi na tano…

34. **MPOKEZI: (clears throat)** Uuuhm nafikiri ana haraka kidogo

35. **METOGBA: (with a finality)** Dakika kumi na tano... akiweza atasubiri, kama hawezi anaweza kuondoka.

36. **SFX: TELEPHONE RECEIVER BEING PLACED BACK**

37. **NARRATOR:** Mpendwa msikilizaji, najua unajiuliza huyu mchezaji maarufu ni nani kwani hata haogopi kumueleza mheshimiwa Makemba amsubiri. Na mie pia nimejiuliza hilo ila jibu linakuja.... Wakati dakika zilikuwa zinapita kwenye ukumbi wa wageni muhimu, kwengineko kwa Shangazi Lily, Safina hakukifahamu kilichomsubiri!

**<u>SCENE FOUR: LATE EVENING AT AUNT LILY'S</u>**

38. **SHANGAZI LILY: (In a hurried voice)** Safina! Nisaidie kuifunga zipu ya hili rinda... chap chap basi nawe, nachelewa kazini!

39. **SFX: ZIPPER BEING ZIPPED UP**

40. **SHANGAZI LILY: (Catching breath)** Aii, itanibidi nifanye bidii niuupunguze huu mwili, lakini hebu niambie, wanionaje, nimependeza?

**41. SAFINA: (very timid voice)** Ndio, shangazi Lily, lakini hili rinda si fupi mno… kwani waenda wapi? Unafanya kazi gani huko?

**42. SHANGAZI LILY:** Hebu, taratibu! Kwanza, sikukuuliza maoni kulihusu rinda langu. Pili, sipendelei maswali yako mengi, sawa? Ukumbuke kufunga kufuli na tumbuu zote, namaanisha zote!

**43. SAFINA:** Naogopa, shangazi Lily, ninaogopa kubaki hapa peke yangu. Sijawahi kuachwa nyumbani peke yangu.

**44. AUNT LILY:** Hakuna cha kukuogopesha... wewe fanya nilivyokwambia... usifungue mlango mpaka utakaposikia sauti yangu... kwa heri. Ukihisi njaa, pasha chakula moto, ule.

**45. SFX:CLICK-CLACKING OF HIGH HEELS**

**46. SAFINA:** Kwa heri shangazi Lily.

**47. SFX: BOLTS AND LOCKS BEING LOCKED**

**OUTRO**

48. **NARRATOR:** Safina anaufunga mlango, akiwa na maswali mengi kuhusu anakokwenda Shangazi yake. Upweke umemzidia jijini Tambarare na anatamani sana kucheza kandanda jambo ambalo hajalifanya kwa muda sasa. Na mpaka hapo tumefika mwisho wa kipindi hiki cha pili "**Mchezo mchafu na mchezo msafi"**,katika makala ya **"Kabumbu Afrika - ni zaidi ya mchezo".** Usikose kujiunga nasi katika kipindi kijacho utakapomjuwa mchezaji huyo maarufu na atakavyolipokea ombi la mheshimiwa Makemba. Kumbuka Chedede pia anajiandaa kwenda kwenye kliniki hiyo, je itakuwaje baada ya kumueleza Komora? Ukitaka kukisikiliza kipindi hiki au chengine kilichotangulia tembelea kurasa za tovuti zetu: www.dw-world.de/lbe. Mpaka wakati mwengine. Kwa heri!